**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU – TAMISEMI**

**Namba za Simu…………………..**

**Mkuu wa Shule 0764760360**

**Makamu Mkuu wa Shule 0767296983**

**Matron/Patron 0684232579**

**Shule ya Sekondari JENERALI**

**DEVID MSUGULI (NYAILIGAMBA)**

**S.L.P 1523**

**Tarehe ..........................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI JENERALI DAVID MSUGULI (NYAILIGAMBA) HALMASHAURI YA MULEBA MKOA KAGERA MWAKA .................**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2025 na atasoma tahasusi ya …….……

Shule ipo mkoa wa Kagera Wilaya ya Muleba umbali wa km 40 tu kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Muleba barabara iendayo Bukoba mjini kituo cha Magari Muhutwe na barabara inayoenda kamachumu Km 1 kutoka kwenye rami barabara iendayo Kamachumu utaona kibao cha Shule .

Kwa wale wanaotoka Bukoba mjini kwenda Muleba wateremkie Muhutwe na wale wanaotoka nje ya mkoa wa Kagera kupitia barabara ya Biharamlo kuelekea bukoba mjini wateremkie kituo chamagari Muhutwe. Kutoka Muhutwe stendi utaelekea barabara ya kamachumu Km 1 kutoka hapo kwa kutumia bodaboda. Nauli ya bodaboda ni shilingi mia tano hadi elfu moja tu. Shule inayo miundo mbinu ya Umeme pamoja naMaji.

Muhula wa Masomo utaanza tarehe ............. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni ndani ya wiki ya mwezi julai.

**1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**1.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii: ni sketi nyeusi Linda box kubwa, mbele na nyuma kama inavyoonekana hapo chini iwe ndefu iguse vifundo vya miguu na shati nyeupe mikono mirefu
ii. Mashati mawili(02) mikono mirefu.
iii. Hijab (kijuba) rangi nyeupe (02) na zambarau (02) ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.
iv. Sare ya Michezo ni Bukta ya blue, tisheti nyekundi na raba nyeupe
v. Track suit nyekundu
vi. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vii. Raba za michezo rangi nyeupe
viii. Soksi jozi mbili nyeupe za shule;
ix. Aje na T-shert ya bluu yenye kola, T-shert ya zambarua(puple) ya round na sweta ya bluu. **KAMA HATAZIPATA** zinapatikana karibu na mazingira ya shule kwa kiasi cha Tshs. 40,000/= kwa vyote vitatu.
x. Tai nyeusi moja (01)

i. Nguo za kushindia ni Sketi ya zambarau mshono ni linda box.mshono uwe hivi



**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari kumi (10) Quire 3
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka,***aina ya Double A***
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha iambatishwe*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator;
vi. Godoro 2½
vii. Mashuka Jozi 02 rangi ya blue, blanket 01, foronya ya godoro 01, chandarua 01 na mto 01.
viii. Nguo za ndani za kutosha, taulo pamoja na kitenge kimoja.
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
*x.* Ndoo 02 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja 01, mopa(squizer) 01, fagio 01(soft broom) kwa michepuo ya **PCB** na **CBG,**
xii. jembe 01, mopa(squizer) 01 na fagio (chelewa)01 kwa michepuo ya **HGK, HGL HGFa, HGLi na HKL**. kutokana na umbali vifaa hivi unaweza kuvipata karibu na mazingira ya shule.
xiii. Mwanao anatakiwa aje na bima ya afya kwa ajili ya matibabu yake kama hana bima ya afya alete fedha kwa ajili ya kukatiwa bima ya afya kwa mwaka mmoja.

ORODHA YA VITABU MWANAFUNZI WA KIDATO CHA TANO ANAVYOTAKIWA KUWANAVYO (ITAKUWA NI MALI YAKE)

| SOMO | JINA LA KITABU | MWANDISHI | TOLEO | MAONI |
|---|---|---|---|---|
| CHEMISTRY | 1.A-Level Chemistry | E.N Remsden | 4th Edition | -Topiki zote |
| | 2.Physical | Mark Daniel | | General & |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Chemistry | | | Environmental chem. |
| | 3.Inorganic Chemistry | Mzumbe books project | Part I and part II | Soil & Environmental chem. |
| PHYSICS | 1.Principle of physics for class XI | V.K Mehta (S. Chand) | Revised Edition | |
| | 2. Principle of physics for class XII | V.K Mehta (S. Chand) | Revised Edition | |
| | 3.University physics with Modern Physics | Young and Freedom | 12$^{th}$Edition | |
| | *4.Advanced Level physics* | Tom Duncan | 4$^{th}$Ed. | |
| | *5.Advanced Level physics* | Nelkon &Parker | 5$^{th}$&7$^{th}$Ed | |
| | *6. Advance Level Physics* | Roger Muncoster | | |
| BIOLOGY | 1.Biology science | R.SOper | 3$^{rd}$Edition | |
| | 2.New understanding Biology | P.O.GREEN & Nelson Thomas | Third edition 4$^{th}$edition | |
| ADV.MATHS | 1.Understanding pure math | A.J.Sadler | | |
| | 2.Mathematics for class X I | S.Chand | | |
| | 3.Mathematics gor class XII | S.Chand | | |
| HISTORY | 1.Mastering Adv. Level.PP.I | Kato, A. | 2$^{nd}$ed. | |
| | 2.Oxford Advance Learners | | 1$^{st}$ed. | |
| | History | Oxford | 1$^{st}$ed. | |
| | 3.History Part II | Zisti,K | | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Alive | | | |
| GEOGRAPHY | 1.Monkhouse 9pysics Geography) | Monkhouse | | |
| | 2.Geography an integrated | David Waugh | | |
| | 3.Approved 4th ed. | | | |
| KISWAHILI | Kiswahili 1, Nadharia ya lugha, Kidato cha 5&6 | By Masuko Christopher | | |
| | 2.Kiswahili 2,Nadharia ya Fasihi Kidato cha 5&6. | | | |
| | 3.Tasfiri na ukalimani | By Pr. Mansoko | | |
| BAM | 1.Pure and Applied Math`s | C.J.Tranter | | |
| | 2.Advance Math 1 | C.W.Celia | | |
| GENERAL STUDIES | 1.General studies Notes | -Nyambari C. Nyangwine.Godfrey R. Bukagile 7 Stephen O. Maluka -2009 | | |
| | 2.General studies supplementary book for A-level and Colleges | Civic education Teachers association (CETA)-2010 | | |
| ENGLISH | Advanced English Language Form 5&6 | James John (Oxford univ.press | 1st Ed. | |

NB:Mwanafunzi apate Kimoja kila somo kulingana na TAHASUSI YAKE

### 1.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Malipo yafanyike kupitia A/C NO. 32001200059 JINA LA ACCOUNT NI MDC NYAILIGAMBA SECONDARY SCHOOL.**

**2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na

Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;

iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xix.

**AHADI YA MWANFUNZI KWA UONGOZI WA SHULE**

Nimezisoma Sheria /Kanuni hizi na kuzielewa nitazitimiza .

Jina la Mwanafunzi…………………………………………………………………………

Sahihi ya Mwanafunzi……………………………………………………….

Jinala Mzazi/Mlezi ……………………………………………………………………………….

Tarehe ……………………………………………………………………………………….

**IJAZWE NA MZAZI/MLEZINA KURUDISHWA SHULENI**

ANWANI YA MLEZI
……………………………
……………………………
TAREHE…………………

**KUMB NA………………………………..**
MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI JENERALI DAVID MSUGULI
S.L.P. 1523,
**MULEBA.**

**YAH: MALEZI YA MTOTO ……………………………………………………..KIDATO CHA………MWAKA……………**

**NIMEZISOMA SHERIA NA** Kanuni za shule Kumb.Na.NYB/SS/01 nakuzielewa.
Ninapenda kuhakikisha kwamba mimi mzazi/mlezi wa mtoto huyo /niko tayari kusaidiana na shule katika jitihada zote za kumjengea mtoto wangu nidhamu ya dhati.
Naahidi nitajitahidi kumwongoza kwenye masomo yake kulingana na taratibu za shule.

**ZINGATIA:**

i. Asikose kuhudhuria shuleni kama hakuna sababu ya msingi ya kumzuia na akikosa, apewe kibali toka kwa mzazi/mlezi wake bila hivyo hatapokelewa.
ii. Asijihusishe na matendo ya utoro, uzururaji, matumizi ya madawa ya kulevya na vitendo vingine ambavyo vinaweza kumzui akuendelea na shule.
iii. Asipuuze au kukataa kuhudhuria miradi ya shule, kama vile kilimo na kutunza usafiwa mazingira.
iv. Asijihusishe na migomo au ushawishi wowote unaoweza kuvunja amani ya shule kwa kufanya hivyo atafukuzwa shule maramoja.
v. Akazaniwe masomo kwa lengo la kufaulu mitihani yake ya ndani na ya nje .

……………………………… ………………………
**JINA KAMILI MZAZI/MLEZI NA SAINI**

## MEDICAL EXAMINATION FORM

DATE…………………… NAME OF STUDENT …………………………………………………

To medical office I/C of ……………………………………………………………. District/Regional;/Referral/Designated

Hospital: P.O.BOX …………………………………………………….
Please examine the above named in full as to his physical and mental fitness for Being able to pursue years of University Studies. In case of an acute defect/disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs.
Eye sight……………………………………………………………………

Heart examination ………………………………………………………..

Blood pressure …………………………………………………………….

Hearing ……………………………………………………………………..

Speech ………………………………………………………………………

Venereal Disease …………………………………………………………..

Leprosy ……………………………………………………………………

Epilepsy ……………………………………………………………………..

Stool routine ………………………………………………………………..

Urine routine ……………………………………………………………

Sickle cell test ……………………………………………………………………

OBP including: ESR………………………………. B/S……………………………

HB…………………………………

Others…………………………………………………………………………

Name……………………………………………………………………………Signature…………………………………….

DESIGNATION……………………………………………………………………………………………………………
OFFICIAL STAMP……………………………………………………………………………………………………….
DATE……………………………………………………………………………………………………………………….

**3. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule ………………………………………**

**Jina la Mkuu wa Shule …………………………………….**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0764760360**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0767296983**
- **Mwandamizi Taaluma 0766287875**
- **Mwandamizi Malezi 0769526863**